

Shirika la Fedha Duniani

Benki ya Dunia pamoja na [Shirika la Fedha Duniani \(IMF\)](#) zilibuniwa mwaka wa 1944 katika mkutano wa viongozi wa duniani Bretton Woods, New Hampshire. Nia ya mashirika haya mawili-yaani "Bretton Woods institutions" kama yanavyojulikana-ilikuwa ni kurekebisha uchumi wa kimataifa baada ya Vita vya Pili vya Dunia. Uwanachama katika Benki uko wazi kwa nchi zilizo wanachama wa IMF.

Shughuli za Benki na Shirika la Fedha zinaingiliana, lakini majukumu yao binafsi yana tofauti kubwa. Benki ya Dunia ni shirika na mikopo lenye lengo la kusaidia nchi zijimudu katika uchumi wa dunia kwa jumla na pia kutilia changamoto ukuzaji wa kudumu wa uchumi-ukuzaji ambao utapunguza umasikini katika nchi zinazoendelea. IMF ina shughuli za kusimamia fedha za ulimwengu kwa kusaidia kuwekwa sawa mipango ya malipo kati ya nchi zote. Pia, hupeana mikopo ya pesa kwa wanachama wenye shida za kutimiza malipo ya mikopo yao. Benki ya Dunia inapopeana mikopo ya kuboresha sera na miradi, Shirika la Fedha Duniani linajishughulisha na sera peke yake. Inapeana mikopo kwa nchi wanachama zenye shida za mda mfupi za kulipa madeni ya kigeni na inajaribu kuorodhesha ubadilishaji kamili wa fedha kati ya wanachama kulingana na mpango wa ubadilishaji usio na vikwazo vingi ulioanzishwa mwaka wa 1973.

Benki ya Dunia hupeana mikopo kwa nchi zinazoendelea ama zile zinazoendelea kubuniwa peke yake, lakini wote [nchi wanachama](#) (masikini na tajiri) wanaweza kutumia huduma na rasilimali za IMF. Ili Shirika la Fedha lifaulu kuendesha shughuli zake vyema, ni muhimu kuwa nyingi ya nchi ulimwenguni zishiriki katika kazi zake. Kwa kuwa biashara na uwezekaji wa kimataifa hazina mipaka, inaelekea kuwa kila nchi inabidi kununua na kuuza pesa za kigeni za kugharamia kuingiliza na kusafirisha bidhaa. IMF husimamia ubadilishaji huu na hujadiliana na wanachama wake juu ya namna ya kuchangia mpango wa fedha ambao uko sambamba ulimwenguni kwote.

Benki ilianza kwa kushughulikia miradi halisi ambayo bado inaendelea kufadhiliwa na shirika hili ambalo pia huepeana mikopo kwa maendeleo ya kawaida ya sera za uchumi. Kati ya matakwa ya kupeana mikopo hii ni kuhakikisha kwamba rasilimali zilizo chache zinatumiwa katika uwekezaji ulio na faida ili kupunguza kuongezeka kwa madeni, kuzuia kuongezeka kwa gharama ya maisha ama kustawisha mashirika ya umma. Kwa kusawazisha namna hii, mikopo ya marekebisho inaweza kusaidia uchumi wa nchi zinazoendelea kuwa na utumiaji wema zaidi wa rasilimali na ndipo kujihakikishia ukuaji bora tena ulio stawi.

Ushirikiano kati ya Benki ya Dunia na IMF ulistawi zaidi mwaka wa fedha wa 2002. Mashirika haya mawili yalipiga hatua za kuvutia kwa kuridhia kuzisameheha madeni nchi masikini zenye madeni makubwa kuambatana na [HIPC Initiative](#) [Mwelekeo wa HIPC]. Mabodi ya Wakurugenzi yali idhinisha mipango ya upunguzaji wa madeni kwa nchi 16 na kujadili namna na jinsi za kupunguza madeni ya nchi 29. Katika mpango wa ushirikiano wao, kila shirika linatilia mkazo shughuli zenye matokeo halisi kwake: IMF inajukumu la majadiliano na almashauri za nchi kuhusu miradi ya mikubwa ya kiuchumi na miradi mengine inayohusishwa. Benki ya Dunia nayo inongoza kwa miradi ya jamii na maswala ya mipango.

Mwezi Agosti 2001 Mabodi ya Benki na Shirika la Fedha walikubali kutilia mkazo ushiriano kati ya Benki na Shirika la Fedha katika miradi ya nchi. Mpango huu una madhumuni ya kutilia nguvu ushirikiano kati ya mashirika haya mawili katika miradi yote ya nchi kwa namna ya kufanya kazi pamoja, kugawanyishiana majukumu kwa kusahilisha shirika linalo ongoza mradi, kutoa ripoti za haki katika majarida ya Bodi ya kila shirika. Hata hivyo kila shirika mwishowe husimamia lenyewe uamuzi wa kutoa mikopo na kuimarisha rasilimali zake. Kulingana na [mradi wa PRSP](#) wa nchi zenye pato dogo zinzosaidiwa na Fund's Poverty Reduction and Growth Facility [Huduma ya Shirika la Fedha ya Kupunguza Umasikini na Kuimarisha Ukuzaji], Benki na Shirika la Fedha zinatazamiwa kufanya kazi pamoja ilikuimarisha utekelezaji wa mpango sambamba wa nchi na pia kuimarisha juhudi zao katika majuku yao. Nchi zenye mapato ya kati zitaandaliwa mipango ya kusimamia mabadiliko katika hali zao inagwa mafanikio yatapatikana na kuimarishwa kwa kushirikiana na kupeana taarifa katika ya Benki na Shirikika la Fedha.

Mengi kuhusu IMF yapatikana: <http://www.imf.org>